

Dira kuu, dhamira, malengo na mbinu ya mradi wa AI4HF



AI4HF


Trustworthy Artificial Intelligence
for Personalised Risk Assessment
in Chronic Heart Failure



AI4HF is funded by the European Union's Horizon
Research and Innovation Programme under Grant
Agreement No. 101080430

Maono

Magonjwa ya moyo na mishipa yanatalia kuwa sababu kuu ya vifo duniani kote; hasa, kushindwa kwa moyo huleta changamoto ngumu katika matibabu, kwani inahusishwa na kutofautiana kwa kiasi kikubwa katika visababishi, madhara yake, na hatari, na matokeo ya baadae ya ugonjwa. Hatari za kiafya za ugonjwa wa moyo kushindwa zinaweza kutofautiana kutoka kwa utendaji duni wa moyo na kulazwa hospitalini mara kwa mara, hadi mapigo ya moyo na kifo.




Kuna haja ya mbinu ya matibabu ya kibinasi ili kurekebisha miundo ya tathmini ya hatari iliyotengenezwa kwa maelezo mafupi ya hatari ya mgonjwa wa moyo kushindwa ili kuboresha matokeo ya mgonjwa. Masuluhihi ya akili ya Bandia yaliyofunzwa kutoka kwa data ya vyanzo vingi vya moyo na mishipa ya damu yana uwezo wa kuchambua sifa sahihi za mgonjwa na kutabiri njia zinazowezekana katika hatua ya awali. Hata hivyo, ufumbuzi uliopo wa Akili Bandia unabakia mbali kutoka kwa kuitishwa kwa matumizi ya kliniki kutokana na kizuizi muhimu: uaminifu wao na kukubalika na madaktari wa moyo na wagonjwa haujapatikana.

Misheni

AI4HF itatengeneza mfumo mpana na sanifu kwa ajili ya maendeleo na tathmini ya Akili Bandia ya kuaminika na ya kimaadili. Suluhisho za AI4HF zitajengwa juu ya seti ya kipekee ya hazina kubwa za data, njia za kuaminika za Akili Bandia na zana za kukokotoa katika magonjwa ya moyo.

Teknolojia hiyo itawezesha kuchambua sifa sahihi za wagonjwa wa moyo kushindwa kutabiri matokeo ya mgonjwa katika hatua za mwanzo za ugonjwa ili kuwezesha matibabu ya wakati na ya kibinagsi.


Tathmini ya washikadau mbalimbali na uthibitishaji wa masuluhisho ya AI4HF itafanywa katika vituo vinane vyakliniki duniani kote. Masuluhisho ya AI4HF yanapaswa kuaminiwa, kuidhinishwa na kutumwa katika ulimwengu halisi kwa manufaa ya wagonjwa, madaktari wa moyo, madaktari, watoa huduma na jamii kwa ujumla.



Lengo na mbinu ya kiutekelezaji

Lengo kuu la mradi wa AI4HF ni, pamoja na wagonjwa na wataalamu wa afya, kubuni, kuendeleza, kutathmini na kutumia muundo wa Akili Bandia na wa kuaminika kwa ajili ya kurekebisha usimamizi wa wagonjwa wenyewe moyo kushindwa. Seti kubwa zaidi ya data kuwahi kutokea ya wagonjwa wa kushindwa kwa moyo kote Ulaya, Amerika Kusini na Afrika itatumwa kutengeneza na kutathmini zana za AI4HF ili kuhakikisha kuwa zinatumika katika makundi yote ya watu, mazingira ya kimatibabu na makundi ya kijamii mbalimbali duniani kote.

Washirika wote wa mradi hushirikiana na kufanya kazi katika mfumo wa fani mbalimbali ili kufikia lengo hili adhimu:





AI4HF

Trustworthy Artificial Intelligence
for Personalised Risk Assessment
in chronic Heart Failure



Netherlands
Heart Institute
INTERNATIONAL CLINICAL
RESEARCH CENTER



UNIVERSITAT DE
BARCELONA



UMC Utrecht



Vall d'Hebron
Institut de Recerca



SRDC

SOFTWARE
RESEARCH & DEVELOPMENT
CONSULTANCY



Amsterdam UMC
Universitair Medische Centra



fighting heart disease
and stroke
european heart network



CERTH
CENTRE FOR
RESEARCH & TECHNOLOGY
HELLAS



Barcelona
Supercomputing
Center
Centro Nacional de Supercomputación



ESC
European Society
of Cardiology



regenold



UNIVERSITY OF
OXFORD



AI4HF is funded by the European Union's Horizon
Research and Innovation Programme under Grant
Agreement No. 101080430